# Bishop Salalah: Notes for a series of lectures on spiritual warfare given at the pastors conference, Sept 2008

# Morogoro Chuo Cha Ujenzi Septe. 22.26, 2008

**Utangulizi**

Somo letu la Biblia litakuwa juu ya mafundisho ya Biblia kuhusu Nguvu za giza. Kusudi la somo litakuwa kumfanya mtumishi wa Mungu ayafahamu mafundisho ya Biblia juu ya nguvu za giza ili aweze kuyalinda maisha yake mwenyewe, lakini pia kutoa huduma inayostahili kwa Wakristo.

**Siku ya Kwanza: Agano la kale linafundisha nini juu ya Nguvu za giza.**

Maneno yanayotumika katika Agano la kale kuelezea Nguvu za giza:

Kumbukumbu la toTorati 32:17 “Shedim” miungu wageni.

Mambo ya Walawi 17:7, 2Nyakati 11:15, Isa 13:21, 34:14 “lilitu” – Mungu wa kike.

Zaburi 91:5 – 6 – maneno “ hofu ya usiku” pahad “ mshale urukao mchana” hez na “tauni ipitayo gizani” dever. Yote haya ni majina ya mapepo.

Isaa 65:11 – Bahati “gad” ni jina la pepo aliyeabudiwa na Wakaldayo.

Majina haya yanaashiria kuwa tatizo la mapepo lilikuwapo kwa wa Israeli. Walivutwa kuabudu miungu mingine na kumwachwa Mungu wa kweli.

**Agano la kale linasema nini juu kutafuta kujua mambo ya usoni kupitia kwa wafu.**

Katika kumbukumbu la Torati 18-10-11, Bwana anatoa amri kuwakataza wana wa Israeli kuwaendea wafu. Mistari mingine Lawi 19:31; 20:6; 20:27. Mfalme Sauli aliwakatilia mbali watu waliojihusisha na mambo ya uchawi na pepo. Mfalme Yosia hali kadhalika aliwafukuza waliojishughulisha na mambo ya mapepo2Fal. 23:24. Kwa upande mwingine mfalme Manase alijiingiza katika shida ya kuwaendea wachawi 2Fal 21:6.

Angalia ISam 28:7-14. Tatizo la Sauli kumwendea mwenye pepo wa utambuzi.
Mungu alifanya nini kwa Waisraeli kujua mambo ya usoni Kum. 18:18f.

**SIKU YA PILI**

**Agano Jipya linafundisha nini juu ya nguvu za giza.**

Maneno yanayotumika katika Agano jipya:

Neno “**daimon**” limetumika katika Matt 8:31, Marko 5:12, Luka 8:29 na Ufu. 16:14; 18:2. Neno hili hutumika kuelezea pepo wachafu. (evil Spirits)

Neno jingine ni “**daimonion**”. Neno hili linapatikana katika Matendo ya Mitume 17:18. Limetumika kuelezea miungu. Nyuma ya miungu wanaoabudiwa na watu, kuna nguvu ya mapepo, angalia pia IKor 10:20-21, Ufu 9:20.

Neno “**deisidamonia**”Hili limetumiwa katika Matendo ya Mitume 25:19 kuelezea “dini’ Angalia pia Mdo 17:22. Neno hili linatumika kuelezea ibada inayofanywa kwa mapepo ama miungu.

**<u>Mapepo katika Injili</u>**

Pamoja na kazi zingine ambazo Yesu alizifanya, aliyakemea mapepo yaliyowatesa wanadamu kwa njia mbalimbali. Kazi hii aliwapa wanafunzi wake pia. Matt 10:1ff. Kuyashinda mapepo ilikuwa sawa na kumshinda shetani mwenyewe Lk 10:17-18,

Yesu kamwe hakupuuza nguvu za mapepo Matt. 17:14-20. Angalia pia Matt 12:24.

Mapepo pia yaliwatumia watu kama vyombo kutimiza matakwa yake (i.e. mapepo) Mk5:5 ff Lk 11:14-15.

Mapepo yalisababisha magonjwa kwa wanadamu. Lk 13:11, 16. Lakini mapepo yalizitambua nguvu za Yesu. Matt 8:29.

**<u>Mapepo katika Kitabu cha Matendo ya Mitume, Nyaraka na ufunuo</u>**.

Filipo katika kuhubiri kwake alitoa mapepo pia. Mdo. 8:7. Upinzani wa Elima mchawi ulichukuliwa kuwa upinzani wa Ibilisi. Mdo 13:10. Katika Mdo 16:16 kijakazi aliyekuwa na pepo wa uaguzi alikuwa kero kwa Paulo na Sila mpaka hapo alipokemewa na Paulo.

Katika IKor 10:20f, Paulo anawaambia Wakristo wa Korintho kuwa kutoa sadaka kwa sanamu ni sawa na kutoa sadaka kwa mashetani. Paulo katika Efe. 6:12 anasema kuwa kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Lakini pia mapepo ni chimbuko la mafundisho ya uzushi. I Tim 4:1

Kitabu cha ufunuo wa Yohana kinatoa kilele cha harakati za nguvu za giza. Kupitia mpinga Kristo, Ibilisi atawafanya watu waache kumwabudu Mungu wa kweli na kuwageukia mashetani Ufu. 9:20

Kufuatana na Ufu. 16:13-14, mashetani watafanya miujiza na kuwavuta watu kuiacha kweli ya Mungu. Harakati za mashetani zitakoma wakati Ibilisi aliye mkuu wao atakapotupwa katika ziwa la moto, ufu. 20:10

Ni wazi kuwa mashetani ni watumishi wa Ibilisi. Huendeleza harakati za Ibilisi kwa njia ya mafundisho ya uongo, miujiza na ahata kusabisha magonjwa kwa watu. Haya yote hufanywa ili kumfanya mwadamu asimwabudu Mungu wa kweli.

**<u>SIKU YA TATU</u>**

Uweza wa Injili uletao mabadiliko katika maisha ya mwanadamu na akufunguliwa toka nguvu za giza.

Upo ulimwengu wa nia ambao huongoza ulimwengu wa mwenendo. Katika maisha ya mwanadamu, badiliko lo lote la kweli lazima lianze na ulimwengu wania. Mwenendo, mambo ambayo huonekana na macho ya watu, hutokana na ulimwengu wa nia, kama hakuna badiliko katika ulimwengu wa nia, basi hakutakuwa na badiliko la kweli katika ulimwengu wa mwenendo.

Anguko la Adamu na Hawa lilianza na ulimwengu wa nia. Mwa 3:1-6. Baada ya anguko la nia, mwendo uliathirika Mwa. 3:8-13.

Mtume Paulo anaonekana kukiri kuwa ulimwengu wake wa nia umeathiriwa na dhambi na hivyo basi, ulimwengu wake wa mwenendo umeathirika pia. Warumi: 7:14ff.

Shetani na majeshi yake anaanza kuteka kwanza ulimwengu wetu wa nia. Angalia Rum 1:18-32.

Injili ya Kristo pia lazima ianze na ulimwengu wa nia. Rum 12:1-2

Mabadiliko ya kweli katika maisha ya mkristo lazima yaanze na ulimwengu wa nia. Kama Kristo, ataweka kiti chake cha utawala katika ulimwengu nia, basi hakuna nguvu nyingine itakayochukua nafasi yake.

Imetayarishwa na,

**Askofu Charles S. Salalah**